# DOYEN PUBLISHERS
## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## MTIHANI WA MWISHO MUHULA WA 1 2025
## GREDI YA 9 – KISWAHILI
*(Kartasi ya 1 - Kiswahili Lugha)*

**Muda: Saa 1 dakika 40**

JINA: ______________________________________________

SHULE: ______________________________________________

KITENGO: ______________________ TAREHE: ________________________

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

a) Andika jina lako, shule, kitengo na tarehe katika sehemu zilizo hapo juu.
b) Karatasi hii ina maswali 50 ya uchaguzi wengi. Jibu MASWALI YOTE katika kijitabu hiki cha maswali.
c) Majibu yote lazima yatolewe kulingana na miongozo ya maswali.
d) Kwa kila swali kutoka 1 hadi 50, kuna majibu manne. Majibu haya yameandikwa A, B, C na D. Kila wakati, moja tu kati ya majibu manne ndio sahihi. Chagua jibu sahihi na uandike kwenye jedwali lililo chini.
e) Fanya kazi zote za kujaribu kwenye karatasi ya maswali.

**JEDWALI LA MAJIBU**

| 1. | 2. | 3. | 4. | 5. | 6. | 7. | 8. | 9. | 10. | 11. | 12. | 13. | 14. | 15. | 16. | 17. | 18. | 19. | 20. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

| 21. | 22. | 23. | 24. | 25. | 26. | 27. | 28. | 29. | 30. | 31. | 32. | 33. | 34. | 35. | 36. | 37. | 38. | 39. | 40. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |

| 41. | 42. | 43. | 44. | 45. | 46. | 47. | 48. | 49. | 50 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

**ALAMA ZA MWANAFUNZI**

| | |
|---|---|
| **Kutoka kwa 50** | |

***Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa. Watahiniwa wanapaswa kukagua karatasi hii ili kuhakikisha kuwa kurasa zote zimepigwa chapa kama ilivyosemwa na hakuna maswali yanayokosekana.***

***Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 1 hadi 10***

Usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi katika maisha ya binadamu. Nchi isiyowahakikisha raia wake usalama hujidhalilisha; ni sawa na kuku ambaye aonapo mwewe, anakimbiza roho yake huku akiwaacha vifaranga wake kuwa kitoweo cha mwewe.

Ukosefu wa usalama hauathiri tu mtu binafsi, bali pia huathiri nchi na majirani zake. Mathalani, vita vya kikabila vinapozuka nchini, raia, kwa kuhofia usalama wao, hukimbilia kwa makabila mengine na hata nchi jirani. Wakimbizi hawa, licha ya kuwa wategemezi wa wafadhili wao, hupoteza hadhi yao kama binadamu, kwani daima mhitaji huwa mtumwa. Isitoshe, katika nchi ambazo ukosefu wa usalama umeshikamiri, uchumi hutetereka. Shughuli nyingi za uzalishaji mali na uwekezaji hugonga mwamba. Wawekezaji wa ndani na nje huhofia kupoteza mali na roho zao. Hali hii hupalilia zaidi makali ya ukosefu wa nafasi za kazi na umaskini.

Maeneo mengi katika nchi zilizo na tatizo la ukosefu wa usalama hukabiliwa na uchechefu wa wafanyakazi. Raia **kindakindaki** wa sehemu hizi hupungua. Si ajabu kupata kwamba katika baadhi ya maeneo, wenyeji hawadiriki kujenga humo, kisa na maana; wanahofia kuchomewa nyumba zao na magaidi wanaodai asilimia kubwa ya fedha ili wasitekeleze uhalifu huu. Matokeo ya haya ni kwamba shughuli za kiuchumi kama vile ufugaji zimeachiwa wachache, hususan wazee ambao hawana hamu ya kuhamia mijini. Hali kadhalika, jamii isiyo na usalama huvuruga misingi ya mshikamano wa kijamii.

Ni dhahiri kwamba wanajamii ambao wanaendeleza vitendo kama vile wizi wa mifugo, unyakuzi wa ardhi, ubakaji, na ulawiti hupalilia zaidi utengano miongoni mwao. Vitendo hivi huzua chuki, kisasi, kutoaminiana, na mara nyingine husababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika hali hii, baadhi ya raia huumizwa, wengine hufa na wengine kuachiwa majeraha ya moyo.

Tatizo la ukosefu wa usalama linapozungumziwa, watu moja kwa moja huwanyooshea vidole polisi na walinda usalama wengine. Raia kwa jumla huwa wepesi kusema, "Tunaisihi serikali ituhakikishie usalama." Jambo la kusikitisha ni kwamba **wanaoiomba serikali kuwahakikishia usalama ndio, kwa mfano, wanaojenga kando ya mito na kujitia katika hatari ya kusombwa na maji**. Wengine wanatarajia serikali kuwahakikishia usalama huku wakiabiri magari yaliyojaa watu pomoni bila kuwazia hatari inayowakabili. Wapo wengine ambao huhatarisha usalama wao kwa kunywa pombe haramu na kuambulia upofu. Wengine nao hula vyakula vyenye kemikali zinazoathiri afya zao. Wapo wengine wanaojitia hatarini kwa kupuuza wito wa serikali wa kuhakikisha kuwa wamejua anayeishi karibu nao, na kwamba wamewaangaza wale ambao wanashukiwa kuwa pingamizi kwa usalama. Isitoshe, kuna wale ambao huhatarisha usalama wao kwa kutumia njia za kijadi za matibabu kama vile akina mama kujifungulia nyumbani bila wakunga maalum; jambo ambalo huhatarisha maisha ya mzazi na mtoto pia. Wengine hushiriki vitendo viovu kama vile utunguaji mimba na kujisababishia vifo.

Ni dhahiri kwamba kudumishwa kwa usalama kunahitaji mehango wa kila mwanajamii. Kama kila mtu angejifunga masomo kushughulikia usalama wake na wa jirani, huenda hakungekuwa na haja ya polisi na hata walinda lango.

1. Kulingana na aya ya **kwanza**:
   A. Mzazi asiyewalinda wanawe hupoteza hadhi yake kama mlezi.
   B. Binadamu asiyepata anachohitaji huathirika anapoachwa na mzazi.
   C. Mzazi mwenye ubinafsi huhatarisha maisha yake kama mlezi.
   D. Binadamu mwenye woga hushindwa kuwadhibiti wanawe kama mzazi.

2. Vita vya kikabila:
   A. husababisha kukimbizana kwa majirani;
   B. huwafanya watu kuwa watumishi wa majirani;
   C. huwafanya watu hupoteza heshima yao;
   D. husababisha kutopatikana kwa mali.

3. Aya ya **tatu** imeonyesha kwamba:
   A. Sehemu zilizo na ukosefu wa usalama hazina wafanyakazi.
   B. Tamaa inasababisha ukosefu wa usalama katika jamii.
   C. Maeneo yenye ukosefu wa usalama hayana majengo ya wenyeji.
   D. Kutokuwepo kwa usalama husababisha kutomiliki mifugo wengi.

4. Kulingana na kifungu, athari za ukosefu wa usalama ni:
   A. kupungua kwa uzalishaji mali, kutokuwa wajenzi;
   B. mifugo michache, kutengana na wazee;
   C. kushukiana, uharibifu wa mali;
   D. kuuawa, kupata vidonda mwilini.

5. Mwandishi amedhihirisha kwamba:
   A. Walinda usalama huelekezewa lawama baada ya uhalifu kutokea.
   B. Wenye magari yaliyojaa kote huhatarisha usalama.
   C. Usalama unahusu kujua wanakotoka majirani wasioaminika.
   D. Utulivu unaonyesha uwajibikaji wa serikali inapohitajika.

6. "***Wanaoiomba serikali kuwahakikishia usalama ndio kwa mfano, wanaojenga kando ya mito na kujitia katika hatari ya kusombwa na maji***."
   Onyesha methali inayoweza kutumiwa kuwaonya watu hawa.
   A. Mti huchongewa na tundaze.
   B. Mto huvunjika kingo iliyo mbovu.
   C. Ukibebwa usilevyelevye miguu.
   D. Ukipanda pantosha utavuna pankwisha.

7. Ni wazi kwamba kudumisha usalama kunahitaji:
   A. raia wenyewe kuyatambua matatizo ya waishio kwao;
   B. wanajamii wenyewe kufahamu mchango wa serikali;
   C. uwajibikaji wa mtu binafsi katika shughuli zake;
   D. kujifunza aina za lishe bora wenyewe.

8. Kulingana na kifungu serikali:
   A. inawataka watu kuwaogopa wanaodhaniwa kuwa wahalifu;
   B. inawashauri watu kuepuka kupata watoto nyumbani;
   C. inawaonya watu dhidi ya mauaji wakiwa wachanga;
   D. inawahimiza watu kujua mienendo ya majirani wao.

9. Wazo **kuu** linalojitokeza katika aya ya mwisho, ni:
   A. Usalama unadumishwa kwa mtu kuishi karibu na nyumbani.
   B. Inamjuzu mtu kuwazia usalama unaoelezewa na wanajamii.
   C. Ni muhimu mtu kujitahidi kuhakikisha usalama kwake na katika mazingira yake.
   D. Maafisa mtaani hawahitajiki pale watu wanapoamini ni salama.

10. Chagua maana ya **kindakindaki** kwa mujibu wa kifungu.
   A. waliozaliwa hapo
   B. waliohitajika hapo
   C. waliopatikana hapo
   D. waliothaminiwa hapo.

***Soma kifungu kilichofuata kisha jibu swali la 11 hadi 20***

Siku hiyo jua lilichomoza mapema kuliko kawaida. Niliitazama miale yake kupitia kwenye dirisha la chumba changu. Rangi ya miale hii iliibua mjadala moyoni mwangu. "Sijui kama macho yangu ndiyo yanayonipiga chenga, ila naona leo miale hii ina mabaka meusi yaliyotwaa wekundu wa damu," moyo wangu ukasema. "Ingawa mimi si mnajimu wala mshirikina, nadhani rangi hii imefumbata kitendawili fulani," moyo ulirudia kusema. Baada ya mawazo haya nilishusha pumzi ndefu na kusema, "Siku njema huonekana asubuhi, huenda hii ni dalili ya wema wenyewe. Juu ya hayo, mustakabali wa siku umo mikononi mwake aliyeiamrisha siku yenyewe kuwepo, bindamu ana hiari au usemi gani kuhusu yatakayokuwa au yatakayokosa kuwepo?"

Nilijikokota kutoka kitandani mwangu. Siku hii nilikuwa na miadi na rafiki yangu Tindi ambaye alihitaji kununua vifaa vya nyumbani. Rafiki huyu alikuwa amepata kazi ya uhasibu katika Shirika la Utozaji Ushuru baada ya

kipindi cha kuhangaishwa na ulaji rushwa. Alikuwa anagura alikoishi na wazazi wake. Kama alivyosema, alitaka kuishi peke yake ili ajifunze kujitegemea. Tulikuwa tumepanga kukutana katika jengo moja la kibiashara ambamo mliuzwa aina nyingi za vifaa vya nyumbani.

Nilifika kwenye jengo hilo baada ya saa moja na nusu. Nilimngojea rafiki yangu kwa takriban saa mbili ingawa alikuwa ameahidi kufika mapema. **Hata hivyo, kuchelewa huku hakukuwa ibra kwangu**. "Vipi Bwana? Leo umezidi?" Nilimuuliza Tindi. "Samahani sana ndugu, ila wewe unajua katika mji wa Selea methali, 'Chelewa chelewa utampata mwana si wako,' haiwezi kuafiki. Hata mtu ukitaka kuchapuka vipi, msongamano wa magari utakutilia vizingiti," alijibu kama kawaida yake.

Tulijitoma katika shughuli ya ununuzi. Mara, "Leta hiki," mara, "Rudisha, hiki ni ghali mno," mara, "Punguza bei." Hata baada ya muda usiopungua saa tano na nusu, tulikuwa tumenunua vyote vilivyokuwa kwenye orodha yetu ya bidhaa. Ghafla taa za umeme zilizimika, mlio wa jenereta ukasikika, kisha mlipuko, na kiza cha kutisha. Mara nilisikia ukemi mkubwa uliopasua dari ya jengo hili. Ukemi huu ulifuatwa na sauti nene ya kiume, "Fungeni vishubaka vya pesa! Nenda kafunge mlango wa mbele na wa nyuma!"

Wakati hayo yote yakijiri, jumba lilikuwa limekumbatiwa na moto wa tanuri. Joshi jeusi lilitanda kila mahali, vilio vya wateja waliokuwa wanatapatapa huku na huko kama kuku aliyedenguliwa shingo viliremba mandhari haya. Nilimshika Tindi mkono na kukimbilia mlango wa nyuma ambamo alisimama mlinda lango mmoja kuhakikisha hatubebi bidhaa yoyote; hata zile tulizokuwa tumelipia. Nilijaribu **kumsihi** atufungulie tutoke lakini akakataa katakata. Amri ya Bwana Mkubwa ilimzuia hata kuona hatari iliyomkabili yeye. Hatimaye nilifanikiwa kutumia misuli yangu kumwondoa, nikajishukuru kwa mazoezi ya viungo ambayo mimi hufanya kila siku.

Mimi na Tindi tulifanikiwa kutoka nje bila majeraha ya haja. Ndani kule vilio vya roho zilizokuwa zikibanania kwenye mlango wa nyuma vilihanikiza. Bwana Mkubwa alikataa katakata kufungua mlango wa mbele; anahofia mali yake kukwepuliwa na wafu! Wapo walionusurika, wakapitia kwenye mlango huu, wapo waliosalimu amri ya moto, moshi, hewa yenye sumu na kubanwa na wenzao. Hata Shirika la Zimamoto lilipowasili baada ya saa nne, jengo hilo lilikuwa majivu pamoja na vyote vilivyokuwemo. Runinga ya Taifa usiku huo iliarifu kwamba **hata mwenye jengo aliyesimama wenye mlango wa mbele kulinda mali yake dhidi ya roho zilizokuwa zinateketea aliaga dunia**.

11. Miale ya jua asubuhi hii:
    A. llionyesha hali ya kuamini uchawi.
    B. Ilimfanya Msimulizi kufikiri zaidi.
    C. Ilikuwa kinyume na matarajio ya unajimu.
    D. Ilisababisha upuuzaji moyoni mwa mtazamaji.

12. Aya ya **kwanza** imedhihirisha kwamba:
    A. Jambo huweza kutisha hata kama linaonekana zuri.
    B. Ishara ya yanayotokea huonyesha mafanikio hapo mbeleni.
    C. Binadamu hana mamlaka kuhusu hali inayoyoathiri maisha yake.
    D. Mtu hukosa hakika ya mafumbo anayotoa akilini mwake.

13. Chagua jibu **lisilo sahihi** kwa mujibu wa kifungu.
    A. Msimulizi anajua hii ni mara ya pili Tindi kuchelewa.
    B. Ufisadi huathiri utoaji wa ajira nchini.
    C. Kuwepo kwa magari mengi barabarani hutatiza shughuli.
    D. Pesa humpa mtu nafasi ya kufurahia uhuru wa kibinafsi.

14. Kauli, "***Hata hivyo kuchelewa huku hakukuwa ibra kwangu***", inamaanisha:
    A. Aghalabu Tindi hazingatii muda waliokubaliana kuanza shughuli.
    B. Tindi ana hulka ya kuchelewa anaponunua bidhaa.
    C. Msimulizi amezoea kutotimiza miadi ya Tindi
    D. Ni kawaida kwa Msimulizi kumwona Tindi baada ya kuchelewa.

15. Chagua mfuatano ufaao wa matukio kulingana na taarifa.
   A. kuagiza bidhaa, kujadiliana bei, kupotea kwa umeme, mpasuko, giza nene.
   B. kuagiza bidhaa, kukagua bidhaa, kuagiza nyingine, kupotea kwa umeme, sauti, giza nene.
   C. kuagiza bidhaa, kununua vyote, kupotea kwa umeme, moshi, giza nene.
   D. kuagiza bidhaa, muda kuyoyoma, vilio, kupotea kwa umeme, giza nene.

16. Chagua sifa **kuu** za mwenye jengo kulingana na kifungu.
   A. mwenye pupa, mwoga
   B. mwenye tamaa, asiyewajibika
   C. mwenye wivu, katili
   D. mwenye dharau, asiyeamini

17. Chagua jibu ambalo **si sahihi** kwa mujibu wa kifungu.
   A. Maafa mengi husababishwa na kutowazia hatima za matendo yetu.
   B. Utiifu huweza kumletea mtu madhara.
   C. Desturi katika maisha yetu huweza kutuletea neema.
   D. Sheria zitolewazo wanapoiba huweza kudhibiti waokoaji.

18. Aya ya **mwisho** imebainisha kwamba:
   A. Msimulizi na Tindi walinusurika kuumizwa.
   B. Watu wengi walikufa kwa sababu ya kulinda mali zao.
   C. Uharibifu mkubwa ulisababishwa na kutochukua hatua haraka.
   D. Kufinyana kwenye moto kulileta moshi na sumu.

19. Chagua kisawe cha **kumsihi**.
   A. kumrai
   B. kumwelekeza
   C. kumtahadharisha
   D. kumshauri

20. "***Hata mwenye jengo aliyesimama kwenye mlango wa mbele kulinda mali yake dhidi ya roho zilizokuwa zinateketea aliaga dunia***."
   Chagua tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika kauli hii.
   A. tashbihi, sitiari
   B. kinaya, nahau
   C. ishara, tashihisi
   D. chuku, majazi

***Kifungu kifuatacho kina nafasi 21 hadi 28. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kujaza nafasi.***

Mazungumzo ___**21**___ kanuni fulani ili ___**22**___ Lugha ___**23**___ msemaji lazima ___**24**___ na msikilizaji, ___**25**___ sivyo kuwasiliana hakutapatikana. Mtu ___**26**___ kuzungumza huanza kwa kutamka sauti. ___**27**___ sauti hizi huwa ghuna. Mfano wa sauti ghuna ni ___**28**___.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 21. | huzingatiwa | huzingatiana | huzingatia | huzingatisha |
| 22. | kuzifanikisha | kumfanikisha | kuyafanikisha | kuifanikisha |
| 23. | anayotumia | anapotumia | anaotumia | anavyotumia |
| 24. | ueleweke | aeleweke | lieleweke | ieleweke |
| 25. | lau | tena | bali | wala |
| 26. | akijifunza | amejifunza | akajifunza | anajifunza |
| 27. | baadhi ya | mithili ya | zaidi ya | licha ya |
| 28. | m, f, g, th | v, z, dh, w | ch, s, d, t | n, gh, h, k |

***Kutoka swali la 29 hadi la 50 chagua jibu sahihi.***

29. Kamilisha sentensi kwa kutumia kihusishi cha mahali:
Ndege wametua ________ miti iliyopandwa na rais.
A. baada ya
B. hadi
C. juu ya
D. miongoni mwa

30. Chagua aina za maneno yaliyopigiwa mstari.
Wageni **wale** walialikwa tena lakini wengine hawakualikwa.
A. kivumishi, kielezi, kiwakilishi
B. kiwakilishi, kihusishi, kielezi
C. kielezi, kihusishi, kiwakilishi
D. kihusishi, kivumishi, kielezi

31. Kauli zilizopigiwa mstari zimetumia tamathali gani za usemi?
Wanjiku ni chiriku anaweza kutamka maneno mia moja kwa sekunde.
A. majazi, nahau
B. tasfida, kinaya
C. sitiari, chuku
D. tashbihi, ishara

32. Sentensi ipi ni sitiara?
A. Mohamed ni mpole kama njiwa.
B. Keith ni shujaa kama simba.
C. Rudisha ni mlingoti.
D. Ursula ana mbio kama duma.

33. Chagua **jibu lisilolingana** na mengine.
A. unga – kata
B. laini – ngumu
C. kumbuka – sahau
D. imara – thabiti

34. Chagua sentensi yenye "ki" ya wakati.
A. Wachezaji wanaimba wakishangilia.
B. Kikataa hicho kililimwa kikatoa mazao mengi.
C. Fundi alikishona kitambaa vizuri.
D. Wafanyakazi wanaifanya kazi hiyo kivivu.

35. Onyesha kauli ya kutendea ya sentensi zifuatazo:
Munga alitengeneza gari. Munga alikuwa kiwandani.
A. Munga alitengenezea gari kiwandani.
B. Kiwandani walimtengenezea Munga gari.
C. Munga alitengenezewa gari kiwandani.
D. Kiwandani kulitengenezewa gari la Munga.

36. Chagua sentensi yenye maelezo sahihi.
A. Kukoga ni kuondoa uchafu mwilini na kukonga ni kutawanyia vitu mahali.
B. Kufuta ni kusukuma kitu kuelekea uliko na kuvuta ni kunusa.
C. Kusuka ni kutikisa kitu ilhali kuzuka ni kutokea kwa jambo.
D. Kutunga ni kupitisha uzi mahali ilhali kudunga ni kutoboa shimo.

37. Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.
A. Lo, huoni unamzuia mwenzako?
B. Heza -alisema - Koru tutakutanakesho.
C. Mugou (yule mtangazaji hodari) amepata Tuzo ya Mtangazaji Bora.
D. Yafuatayo ndiyo yanayotarajiwa, kusajiliwa, kulipa karo, kuanza masomo.

38. Chagua sentensi ambayo inaunganisha sentensi zifuatazo ipasavyo.
Gari lilikuwa jipya. Gari halikumpendeza.
A. Gari lilikuwa jipya madhali halikumpendeza.
B. Licha ya gari kuwa jipya, halikumpendeza.
C. Gari lilikuwa jipya angaa halikumpendeza.
D. Mithili ya gari kuwa jipya, halikumpendeza.

39. Eleza maana ya maneno yaliopigiwa mstari:
Mfanyakazi aliyekiuka maadili **amepigwa kalamu**.
A. Mfanyakazi amekubaliwa tena kazini.
B. Mfanyakazi amepigwa kichwa kwa kosa lake.
C. Mfanyakazi amefutwa kazi.
D. Mfanyakazi amepewa onyo kali.

40. Wingi wa, "Ua wa nyumba yake umejengwa na fundi mwenye bidii," ni:
A. Ua wa nyumba zake umejengwa na mafundi wenye bidii.
B. Nyua za nyumba zao zimejengwa na mafundi wenye bidii.
C. Nyua za nyumba zao zimejengwa na fundi mwenye bidii.
D. Ua wa nyumba zao umejengwa na fundi mwenye bidii.

41. Neno, ‘**kiliundiwa**’ lina silabi ngapi?
   A. 3
   B. 4
   C. 5
   D. 6

42. Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya **I-ZI** pekee.
   A. pamba, taa
   B. kucha, sahani
   C. kuta, ngoma
   D. nyuta, kamba

43. Ni jibu lipi lenye maelezo **sahihi**?
   A. Kipaji ni sehemu ya kichwa inayohifadhi ubongo.
   B. Goti ni sehemu ya mguu inayounganisha muundi na wayo.
   C. Kiwiko huunganisha kiganja na sehemu ya juu ya mkono.
   D. Ufizi ni mfupa uliopo baina ya mdomo wa juu na wa chini.

44. Chagua **ukanusho** wa:
   Maembe yalitiwa kapuni yakaiva.
   A. Maembe hayajatiwa kapuni na hayaivi.
   B. Maembe hayakutiwa kapuni wala hayakuiva.
   C. Maembe hayakutiwa kapuni yaive.
   D. Maembe hayajatiwa kapuni yakaiva.

45. Sentensi ipi ina **kiwakilishi cha nafsi**:
   A. Nyinyi mlijua kwamba mtacheza mechi kesho?
   B. Yule ni mtalii kutoka Uingereza.
   C. Kile kilikuwa kinywaji chenye ladha nzuri.
   D. Lile ni mti wa zamani uliojaa historia.

46. Chagua jibu lenye nomino iliyoundwa **kutokana na nomino**.
   A. angaza – mwanga
   B. samehe – msamaha
   C. babaika – babaifu
   D. mpishi – mapishi

47. Usemi wa taarifa wa, "Mtavihifadhi vitabu vyenu kwenye kabati," mwalimu akatuambia, ni:
   A. Mwalimu alituambia kwamba tutavihifadhi vitabu vyetu kwenye kabati.
   B. Mwalimu alituambia kwamba tungevihifadhi vitabu vyetu kwenye kabati.
   C. Mwalimu alituambia kwamba tumevihifadhi vitabu vyetu kwenye kabati.
   D. Mwalimu alituambia kwamba tulivihifadhi vitabu vyetu kwenye kabati.

48. Andika katika **hali ya mazoea**:
   Mwalimu anasahihisha vitabu.
   A. Mwalimu anasahihisha vitabu.
   B. Mwalimu husahihisha vitabu.
   C. Mwalimu alisahihisha vitabu.
   D. Mwalimu atahakikisha vitabu.

49. Chagua sentensi isiyo na **-ki- ya masharti**:
   A. Watu wakitumia teknolojia wataweza kuchimba madini.
   B. Makiwa kwa shabiki aliyefiwa.
   C. Tukipanda miti mingi, viwango vya mvua vitaongezeka.
   D. Mkulima huyu akitumia mbolea ifaayo, atapata mazao mengi.

50. Nilipotoka nje, kulikuwa na giza ___________
   A. Toronto
   B. totoro
   C. tororo
   D. toro

## HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA